# HALMASHAURI YA MJI MASASI

## MJI WETU-FAHARI YETU

Jarida la Mtandaoni | *Toleo na. 1* / *www. masasitc.go.tz* | Julai-Septemba 2023

## YALIYOMO


- **Nendeni mkasikilize na kutatua kero za wananchi.** *Uk. 2*



- **"Wanamasasi jiungeni na huduma ya Umeme kwa wingi " Mhe. Mwambe** ***Uk.3***
- Wananchi wamshukuru Rais Dkt. Samia Ujenzi Shule Mpya. *Uk. 6*
- **Masasi Mji yapata Makamu Mwenyekiti Mpya.** ***Uk. 8***
- Mkurugenzi mpya **Ndg. Jichabu** akabidhiwa rasmi ofisi, Mwenyekiti Halmashauri na Mbunge watoa Neno ***Uk.10***
- **Watoto zaidi ya 200 wapata elimu ya lishe, wanaume jitokezeni..** *Uk. 12*
- **Makala:** Ziara ya Dkt. Samia "Yaifungua" Masasi Mji na Kuleta "Nuru" kwa Wananchi. ***Uk.13***
- **Michezo: Mapokezi ya Mabingwa wa Mpira wa Wavu Afrika Mashariki.** *Uk. 15*


*Tembelea Tovuti yetu kupata Nakala yako/www.masasitc.go.tz*

# NENDENI MKASIKILIZE NA KUTATUA KERO ZA WANANCHI




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka Viongozi wa ngazi zote kwenda kusikiliza na kutatua kero za wananchi na kuacha tabia ya kukaa maofisini.

Mhe. Rais Samia ametoa maagizo hayo Septemba 17, 2023 wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa Boma uliopo Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara .

Ameeleza kusikitishwa kuona kero za Wananchi wa Vijijini zinafika mpaka Ikulu wakati kwenye maeneo yao kuna Viongozi wa ngazi zote.

Mhe. Rais amesema, "Nitoe wito kwa Uongozi mzima wa Mkoa na ngazi zote hadi Uongozi wa Vijiji na Mtaa kusikiliza na kutatua kero za Wananchi, Waziri wa TAMISEMI amelisema vizuri hapa nami naomba nimuunge mkono, mtakaposhuka jamani, nyinyi sio Watawala, hata Mimi sio Mtawala, Mimi ni Mtumishi wa Wananchi, Mawaziri wangu ni Watumishi wa Wananchi, tuliowashusha chini huku kutuwakilisha ni Watumishi wa Wananchi"

"Unapoacha kiti cha Utumishi ukakaa kiti cha Utawala ndio maana huwezi kushuka kwa Mwananchi kwenda kumsikiliza, niombe sana Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) simamieni hilo, Serikali hii mmeiweka nyinyi sasa mkijifanya wadogo na kufanya Watendaji kuwa wakubwa mnakosea, wasimamieni Watendaji warudi wakasimamie Wananchi"

Amesema haivumiliki kero za wananchi kufika ngazi za juu wakati kuna viongozi katika kila ngazi.

"Haipendezi kuna wasimamizi wa shughuli za Wananchi ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata mpaka Vijiji lakini unapokea pale Ikulu kero ya Mwananchi wa Kijiji inakuja kule Ikulu, haipendezi, tuliowaweka kwenye ngazi hizo mna kazi gani!?, kaeni vizuri fanyeni kazi zenu vinginevyo hatutowavumilia kupokea tena kero za Wananchi kule Ikulu wakati huku kuna Viongozi wapo" *Inaendelea..uk 3.*

..Mhe. Rais Samia amehitimisha ziara yake aliyoifanya katika mkoa wa mtwara kuanzia Septemba 14, hadi Septemba 17, 2023 ambapo amezindua miradi mbalimbali muhimu ikiwemo ya afya, maji, barabara na kuzungumza na wananchi katika maeneo yote.

## "WANAMASASI JIUNGENI NA HUDUMA YA UMEME KWA WINGI" MHE. MWAMBE





Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe Geoffrey Mwambe amewasisitiza wananchi wote wa Jimbo la Masasi Mjini kujiunga kwa wingi na huduma ya umeme pale miundombinu ya umeme inapofika katika maeneo yao ili waweze kukuza uchumi wao binafsi na Serikali.

Mhe. Mwambe ameyasema hayo Septemba 22,2023 katika hafla ya kuwasha umeme vijijini kupitia mradi wa REA III, mzunguko wa pili katika Kijiji cha Chakama Kata ya Matawale na Kijiji cha Namikunda Kata ya Mumbaka Halmashauri ya Mji Masasi katika hafla iliyoongozwa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga.

"Natamani kila mwananchi wa jimbo langu aunganishiwe huduma ya umeme ili kukuza uchumi wa mtu binafsi lakini pia ili Tanesco wajuwe kuwa wanawateja wengi ili mapato yao yaongezeke yawe yakutosha na wao waweze kuhudumia Miundombinu ya Serikali ambayo imewekwa"
Mhe Mwambe

Aidha Mwambe amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza Nguzo 40 za umeme kwa kila kijij, ambazo zinamaliza kabisa tatizo la upungufu wa nguzo katika

Inaendelea... uk 4

vijiji hivyo. “kwanza wananchi wangu tunabahati sana Mhe.Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongeza nguzo 40 kwa kila kijiji ili kuhakikisha huduma ya umeme inawafikia wananchi wote” Mhe. Mwambe

Kwa upande wake, Naibu waziri wa Nishati Mhe.Judith Kapinga ameeleza kuwa Serikali imetoa Bilioni 98 kwa ajili ya kusambaza umeme katika Halmashauri zote tisa za Mkoa wa Mtwara na Halmashauri ya Mji Masasi wametumia zaidi ya billion moja na Mkandarasi yuko saiti.

“Serikali imetumia zaidi ya bilioni moja kwa Halmashauri ya Mji Masasi kutengeneza miundombinu ya umeme na Mkandarasi yuko saiti na lengo letu Masasi Mji tunaenda kuunganisha na Gridi ya Taifa ,tunamshukuru Mhe. Rais na tunategemea ndani ya miezi 18 mpango huu utakuwa umekamilika hivyo natoa rai kwa wananchi wote kuwa na muamko wa kuvuta Nishati hii katika Nyumba zao ” Mhe Kapinga

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Mhe. Lauter John Kanoni amesema watahakikisha wananchi wanaitumia vyema fursa ya kuunganishiwa umeme vijijini kwa shilingi 27000 kwa kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwa na umeme majumbani.




Mkuu wa Wilaya Mhe. John Kanoni akizungumza na wanachi katika hafla ya uzinduzi wa umeme vijijini



Wananchi Kijiji cha Chakama Kata ya Matawale wakishangilia mara ya umeme kuwashwa rasmi.

# "TEKELEZENI WAJIBU WENU KWA UFANISI" MHE. NAMTUMBA



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi, Mhe. Hashim Namtumba amewataka wakuu wa idara, vitengo na wataalamu kutekeleza wajibu wao kwa weledi na ufanisi ili kuchochea maendeleo ya halmashauri.

Amesema wataalamu wanatakiwa kuwa na uhalisia katika ukadiliaji wa fedha katika miradi ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati.

Mhe. Namtumba amesema hayo Agosti 3, 2023 katika mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya nne 2022/2023 uliofanyika katika ukumbi wa Jengo la Utawala.

"Mkurugenzi hoja hapa tuliyonayo ni kwamba hatujawahi kuona fedha zinabaki kwenye mradi, kila mradi fedha hazitoshi hasa miradi inayotekelezwa na fedha kutoka serikali kuu" Mhe. Namtumba

Aidha amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri kwenda kusimamia eneo la ukamilishaji wa miradi ili kuondoa changamoto ya kutokamilisha kwa wakati miradi iliyokwisha tengewa fedha.

"Mkurugenzi hili ni baraza lake la kwanza ni vizuri sasa tukianza pamoja ili turuke pamoja, ukasimiamie eneo la ukamilishaji wa miradi ili tusiwe na miradi isiyokamilika" amesema.

Mkutano wa baraza hilo ulihudhuriwa na waheshimiwa madiwani, wakuu wa idara na vitengo, wakuu wa taasisi mbalimbali, viongozi kutoka vyama mbalimbali, viongozi kutoka ofisi ya mkuu wa mkoa na wadau mbalimbali.

Mikutano ya Baraza la madiwani ni mikutano ya wazi hivyo wananchi wote wa maeneo husika hutakiwa kuhudhuria ili kujionea utekelezaji wa maendeleo.

## WANANCHI WAMSHUKURU RAIS SAMIA UJENZI SHULE MPYA



Uanzishwaji wa shule mpya ya msingi ya mkondo mmoja Mkomaindo iliyopo katika mtaa wa Darajani utapunguza msongamano wa wanafunzi, utoro pamoja na kutembea umbali mrefu wa kwenda shule mama ya awali.

Imeelezwa kuwa baada ya vikao vya kamati mbalimbali ambavyo vilihusisha wananchi waliamua kuwa shule hiyo ijengwe mtaa wa Darajani ili kusogeza huduma za kijamii na hasa ukizingatia kuwa Kata hiyo ina shule moja tu.

Hayo yamesemwa Julai 7, 2023 na Mwalimu Mkuu wa shule Mama Mkomaindo, Suzan Mwaya wakati Mkurugenzi Mtendaji wa Mji wa Masasi alipofanya ziara ya kutembelea shule hiyo ambayo imejengwa kupitia mradi wa Boost.

Mwl. Mwaya ameeleza kuwa shule mama ilipatiwa zaidi ya milioni 331 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya yenye mkondo mmoja.

Mwaya amesema kuwa shule hiyo kwasasa ipo kwenye hatua za umaliziaji vikiwa vimebaki vitu vichache na kwamba walipata changamoto kubwa kwenye matundu ya vyoo vya wanafunzi ya awali kwani walishauriwa kuwa hayako sehemu sahihi ikabidi yafukiwe na kuchimbwa sehemu nyingine.

“Namshukuru sana Rais Samia kwa kutuona hata sisi tuliopo pembezoni mwa Tanzania na kuona matatizo tunayopata kwenye uwezeshaji katika sekta ya elimu ,shule ya msingi Mkomaindo ina wanafunzi wengi ambao ni 1,531 kiasi kwamba unakuta darasa moja wanakaa watoto 185 hivyo kushindwa kumfikia hata yule mtoto aliyemwisho kabisa,”amesema.

# "TUMEPATA MAPOKEZI MAZURI " DKT HILDE




Makamu wa Rais Halmashauri ya Enzkreis ya Nchini Ujerumani, Dkt. Hilde Neidhardt amesema wamefurahishwa na mapokezi waliyoyapata Masasi mkoani Mtwara hususani kupelekwa kufanya utalii katika mto Ruvuma na Pori la Akiba Lukwika Lumesule linalosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania.

Amesema hatua za halmashauri za Masasi Mji na Wilaya kuwapeleka kujionea utalii inazidi kuimarisha ushirikiano na mahusiano baina ya Enzkreis na Masasi.

Amebainisha hayo July 23, 2023 mara baada ya kutembelea na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii katika pori la akiba Lukwika Lumesule ikiwemo wanyama, miamba ndani ya mto Ruvuma na pango la Habiba lenye historia ya kipekee.

Naye, Mratibu wa ushirikiano huo kutoka Enzkreis, Bi. Angela Gewiese amesema ushirikiano kati ya Enzkreis na Masasi ulianza miaka 12 iliyopita na umezidi kuimarika zaidi.

"mimi ndiye mratibu wa ushirikiano kati ya Enzkreis, mji wa Masasi, na halmashauri ya wilaya ya Masasi. Ushirikiano huu umekuwepo kwa miaka 12, na nimefurahishwa sana kutembelea eneo la hifadhi ya wanyama ya Lumesule kwa sababu wakati wa ziara yetu ya kwanza mwaka 2013, eneo hili lilikuwa halina kitu chochote. Kwa hivyo, tunavutiwa sana na maendeleo ya hifadhi hii ya wanyama na kushuhudia jinsi mambo yalivyobadilika kwa *Inaendelea..uk 8*

wakati huu, sasa tuna askari wa uhifadhi na jengo la maonyesho ambapo watu wanaweza kuja kutembelea. Ni jambo zuri sana kuona jinsi utalii unavyokua hapa". Bi Angela.

Ujumbe kutoka Halmashauri ya Enzkreis nchini Ujerumani umeongozwa na Makamu wa Rais wa Enzkreis, Dkt. Hilde Neidhardt, mratibu wa shirikiano huo, Bi. Angela Gewiese, Frank Stephan, Dkt. Jannis Hoek, Melissa Gewiese na Dkt. Till Neugebauer.

Ushirikiano baina ya Enzkreis na Masasi umezidi kuimarisha uboreshaji wa miundombinu ya umeme hususani matumizi ya nishati ya jua kwa kutumia sola yanayolenga kuboresha mazingira na miradi mbalimbali inayotekelezwa kutokana na ushirikiano huo.

## MASASI MJI YAPATA MAKAMU MWENYEKITI MPYA



Diwani kata ya Mumbaka Mhe. Hamisi Nikwanya amechaguliwa rasmi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi.

Awali akitangaza matokeo ya uchaguzi katika mkutano wa Baraza la Madiwani wa mwaka, uliofany ika Agosti 5, 2023, Katibu Tawala Wilaya ya Masasi Bi. Fatma Kubenea ambaye ni Mwenyekiti wa uchag uzi huo, amemtangaza Mhe. Nikwanya baada ya kupata kura za ndio.

Mhe Nikwanya amechaguliwa kwa kupigiwa kura za ndio au Hapana kwakuwa alikuwa mgombea pekee wa nafasi hiyo.

"Jumla ya kura zilizotakiwa kupigwa ni 19, kura zilizopigwa ni 16 kura za ndio ni 12 na kura 4 ziliharibika" Mwenyekiti wa uchaguzi Bi. Fatma Kubenea.

Akitoa neno la shukurani Mhe Nikwanya amewashukuru waheshimiwa.. madiwani kwa kumchagua katika nafasi hiyo na kuahidi kuwa *Inaendelea..uk 9*

ataimarisha ushirikiano baina ya madiwani na watendaji wa halmashauri ili malengo ya halmashauri ya mwaka 2023/2024 yaweze kutimia kwa ukamilifu.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti aliyepita, Mhe. Mbaraka Kodo ambaye ni diwani kata ya Nyasa amewashukuru waheshimiwa madiwani na watendaji wa halmashauri kwa kumpa ushirikiano bora katika kipindi chote cha uongozi wake.

Ikumbukwe kuwa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi lina jumla ya madiwani 19, ambapo waheshimiwa madiwani wa kata ni 14, viti maalumu 4 na Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini kama inavyobainisha orodha hapo chini.



| | |
|---|---|
| Mhe. Hashim Namtumba | Diwani Kata ya Jida (Mwenyekiti) |
| Mhe. Hamisi Nikwanya | Diwani Kata ya Mumbaka (M/Mwenyekiti) |
| Mhe. Ally Salvatory | Diwani Kata ya Mkomaindo |
| Mhe. Rashid Liundi | Diwani Kata ya Sululu |
| Mhe. Mbaraka Kodo | Diwani Kata ya Nyasa |
| Mhe. Hamisi Mnela | Diwani Kata ya Matawale |
| Mhe. Asha Millanzi | Diwani Kata ya Marika |
| Mhe. Frank Maranjila | Diwani Kata ya Temeke |
| Mhe. Valerian Mwajombe | Diwani Kata ya Mtandi |
| Mhe. Ismail Kalindima | Diwani Kata ya Migongo |
| Mhe. Bakari Namtubwi | Diwani Kata ya Mkuti |
| Mhe. Nicholaus Mpetula | Diwani Kata ya Chanikanguo |
| Mhe. Sospeter Nachunga | Diwani Kata ya Napupa |
| Mhe. Mussa Millanzi | Diwani Kata ya Mwengemtapika |
| Mhe. Maimuna Chiputa | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Ashura Nalino | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Shakila Lipetelo | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Benadetha Ndemanga | Diwani Viti Maalum |
| Mhe. Geoffrey Mwambe | Mbunge Jimbo la Masasi Mjini. |

# MKURUGENZI NDG. JICHABU AKABIDHIWA RASMI OFISI NA BI. YEGELLA, MWENYEKITI NA MBUNGE WATOA NENO





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan Septemba 23,2023 alifanya uteuzi na utenguzi wa viongozi mbalimbali ambapo alimteua Ndugu, Reuben Sixbert Jichabu kuwa Mkurungenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi.

Ndg. Jichabu aliapishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Septemba 27,2023 katika ofisi ya Mkuu wa mkoa na Oktoba 2, 2023 aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Bi. Erica Yegella amekabidhi rasmi ofisi kwa Mkurugenzi mpya Ndg. Reuben Sixbert Jichabu .

Hafla ya makabidhiano imefanyika katika Ukumbi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji Masasi, ikishuhudiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji, Mhe. Hashim Namtumba, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Viongozi wa Jumuiya ya wafanyabiashara, Wazee wa mila, Wakuu wa Idara na Vitengo.

Katika hafla hiyo, Mkurugenzi mpya wa Halmashauri Ndg. Jichabu amemshukuru Mhe, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini na kumteua kuwa Mkurugenzi wa Mji Masasi huku akiahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa watumishi, viongozi na wananchi wote.

Aidha amesema halmashauri itakwenda kukusanya mapato kwa mujibu wa kanuni, taratibu, sheria na miongozo ili utekelezaji wa miradi ya *Inaendelea..uk 11*

maendeleo uweze kutimia na kukamilika kwa wakati.

"Miradi yote tuliyokabidhiwa tutaifanya kwa kasi na muda uliokusudiwa, tunakwenda kukusanya mapato, ninaomba mnipe ushirikiano, napenda kutumia akili zaidi, halmashauri hii tunahitaji kukusanya mapato ili shughuli za maendeleo ziendelee, tupo tayari kutatua changamoto zote za wananchi"

Kwa upande wake Bi. Yegella amemshukuru Mhe. Rais kwa Kumuamini katika nafasi mbalimbali za uteuzi huku akibainisha kuwa halmashauri inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo fedha ipo kamilifu kama ujenzi wa shule ya Jida, shule ya sekondari Temeke ( nyumba ya walimu 2 in 1), hospitali ya Mkomaindo na shule ya Sekondari ya Wasichana ya Masasi.

Naye, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi Mhe. Hashim Namtumba amemkaribisha Mkurugenzi mpya wa Halmashauri ya Mji Masasi Ndg. Reuben Sixbert Jichabu huku akiahidi kwamba atapata ushirikiano wa dhati kutoka kwa waheshimiwa madiwani katika kuhakikisha halmashauri na wananchi wanapata maendeleo.

Aidha, amesisitiza umuhimu wa Halmashauri kukusanya mapato kwenye vyanzo vinavyo suasua kwa kuwa mapato ni nguzo muhimu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

"Kwenye eneo la mapato Mkurugenzi, nimepitia maeneo na vyanzo vya ukusanyaji wa mapato, na kuona kuwa bado kuna maeneo muhimu ambayo nguvu inatakiwa kuongezeka maeneo hayo ni maeneo ya servise lavy, hotel levy, parking, na ushuru wa madini".

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini Mhe. Geoffrey Mwambe amesema wateuliwa na watendaji wanapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni, taratibu, sheria na miongozo ili kumsaidia Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, waheshimiwa madiwani na Mbunge katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili Masasi mpya ionekane na wananchi wafurahie maendeleo.

# WATOTO ZAIDI YA 200 WAPATA ELIMU YA LISHE, WANAUME WATAKIWA KUJITOKEZA KWA WINGI



Zaidi ya watoto 200 wamepata elimu ya Lishe bora kutoka vijiji vya Mayula na Mbonde kata ya Mwenge Mtapika Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Masasi wakati wa utoaji wa elimu hiyo, Agosti 16, 2023, Afisa lishe wa Halmashauri ya Mji Masasi, Bi. Happiness Mlamka amesema lengo mahususi la elimu hiyo ni kuwakumbusha wazazi, walezi na jamii juu ya umuhimu wa afya na lishe kwa mtoto.

"kipekee kabisa tumekuja kwenye adhimisho la siku ya afya na lishe ya Kijiji. Siku hii imelenga kuwakumbusha wazazi, walezi na jamii kwa jumla juu ya umuhimu wa afya na lishe kwa mtoto lakini pia kwa jamii nzima, mambo yaliyofanyika leo tumetoa elimu juu ya unyonyeshaji wa Watoto kwa miezi sita hadi miaka miwili, lakini pia tumetoa elimu ya makundi Matano ya chakula, namna sahihi ya kuandaa mlo kamili kwa vile vyakula vinavyopatikana katika jamii kwa vitendo" Bi. Mlamka

Aidha amesisitiza umuhimu wa wanaume kuhudhuria matukio ya elimu ya afya na lishe kwa kuwa ni jukumu la wazazi wote kuhakikisha lishe bora inapatikana.

"leo tumepata baadhi ya wanaume, tunaendelea kutoa wito wanaume wote tuendele kujitokeza kwa kuwa zoezi hili ni la wote" Afisa lishe.

Kwa upande wake, Afisa mtendaji wa Kijiji cha Mayula Bw. Alex Mwambwalwa amesema idadi ya wazazi waliofika katika elimu hiyo imefanikiwa kutoka na uhamasishaji uliofanyika na mwamko wa wazazi juu ya..

*Inaendelea..uk 13*

umuhimu wa lishe kwa Watoto.
"Wananchi tulionao hapa wanatoka katika Kijiji cha Mayula na Kijiji cha Mbonde na Idadi ya Watoto waliohudhuria ni takribani Watoto 200"

Mmoja kati ya baba aliyefika akiwa na mtoto wake kupata elimu hiyo, Bw. Samweli Abdalah mkazi wa Kijiji cha Mayula, amewahimiza wazazi wa kiume kujitokeza kwa wingi katika matukio ya elimu za afya na lishe zinazotelewa na watalaamu ili kuwezesha malezi bora ya Watoto.

# MAKALA

## ZIARA YA DKT SAMIA "YAIFUNGUA" MASASI MJI NA KULETA "NURU" KWA WANANCHI

Ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Halmashauri ya Mji Masasi Masasi "Imeifungua" Masasi Mji na kuleta "Nuru" kwa watoto, wakina mama, vijana, wazee, wakulima, wafugaji, wagonjwa na wananchi wote wa Masasi.

Shamrashamra zilianza mapema Septemba 9, 2023 mara baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas Ahmed kutangaza ziara ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba Septemba 14 hadi Septemba 17, 2023 mchana na usiku atahamia mkoani humo.

Ilikuwa ni habari mpya, kubwa na yenye msisimuko kwa wananchi wa Mtwara. Hatimaye Septemba 14, 2023 Mhe. Rais Samia aliwasili rasmi Mtwara na kupokelewa na maelfu ya wananchi wa mkoa huo.

Ujio huo ulizidi kuenea na kusambaa kwa kasi baada ya ratiba ya Mhe. Rais Samia kuonesha atatembelea Masasi Mji.

Maarufu kama "Kariakoo" ya Mtwara kama alivyobainisha Mkuu wa Wilaya ya Masasi Mhe. Lauter John Kanoni wakati akiwatambulisha viongozi akiwemo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Masasi, Mhe. Hashim Namtumba sambamba na Mkurugenzi wa Mji Masasi Bi. Erica Yegella kwa maelfu ya wananchi waliojitokeza katika mkutano wa hadhara wa Rais Dkt Samia uliofanyika katika uwanja wa boma Masasi mjini Septemba 17, 2023.

"Mji huu wa Masasi ni mji wa kibiashara, hapa ni katikati ya maeneo yote, halmashauri zote zinakuja kutafuta mahitaji yao hapa, kariakoo yao ni hapa" anasema Mhe Kanoni.

Mji huu upo kilomita 210 kusini magharibi mwa mkoa wa Mtwara, ukiwa na ukubwa wa hekta 37,920 huku idadi ya watu kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi 2022 ikiwa ni watu 137,585 wanaume wakiwa 65,781 na wanawake 71,804 wakiupamba Mji kwa shughuli za kilimo cha Korosho, ufuta, mbaazi na mazao mbalimbali ya chakula.

Mji huu unafikika kwa urahisi kutoka pande zote za nchi kwani ni makutano makuu ya barabara kuu ya Tunduru-Songea- Lindi-Dar es salaam-Mbeya, Nachingwea-Liwale-Newala- Tandahimba ukipambwa na hoteli za kifahari, masoko ya bidhaa, viwanda na viwanja vya uwekezaji.

Lakini pia, mtandao wa barabara umeimarishwa kama anavyobainisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed Mchengerwa kuwa mtandao wa barabara unaongezwa kutoka kilometa 6.9 hadi kilometa 11.2.

" Wana masasi wanakushukuru sana Mhe. Rais kwa kazi hii ya kuongeza mtandao wa barabara na kuongeza taa za barabarani" anasema Mhe. Mchengerwa. *Inaendelea..uk 14*

Lakini pia, Nuru kwenye sekta ya afya imepatikana kama alivyobainisha Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, Mhe. Geoffrey Mwambe wakati akizungumza kwa niaba ya wananchi wa Masasi.

“Mhe.Rais nakushukuru sana kwa kung’arisha Masasi, Mji unang’aa Mji ni mpya barabara za lami ziko nyingi na zinapendeza na upande wa afya zaidi ya shilingi bilioni 2 umetuletea wanamasasi kwa ajili ya ukarabati wa hospitali yetu ya wilaya Mkomaindo hadi kufikia 2025 hospitali yetu itakuwa mpya”

Aidha, Nuru ikapatikana kwenye sekta ya maji ambapo Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso amesema Serikali itatoa fedha kiasi cha Tsh milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa chanzo cha maji Nangowo ili maji safi ya uhakika na kutosha yapatikane Masasi na maeneo ya pembezoni.

Hatimaye, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt, Samia Suluhu Hassan akahutubia maelfu ya wananchi waliojitokeza katika mkutano huo.

“Nawashukuru sana wananchi wa Masasi kwa kujitokeza kwa wingi namna hii, nashukuru kwa heshima mliyonipa”

Ujio wake katika Halmashauri ya Mji Masasi Masasi “Umeifungua” Masasi Mji na kuleta “Nuru” kwa watoto, wakina mama, vijana, wazee, wakulima, wafugaji, wagonjwa na wananchi wote wa Masasi.

Nuru kwenye “Umeme” Mhe.Rais Samia amesema safari ya kuondoa adha ya kukatika kwa umeme ndani ya Masasi imeanza na Serikali imejizatiti katika hilo.

“ Kwa sasa mkandarasi yupo kazini kuinganisha Masasi kwenye Gridi ya Taifa kutokea Ruvuma. Pia kuna mkandarasi anatoa umeme Ruangwa kupitia Nangugwa, ambao utakuwa tayari ifikapo Desemba mwaka huu. Baada ya miezi 18 umeme wa uhakika utakuwa umefika”.

Nuru kwenye “Kilimo” mfumo wa stakabadhi ghalani umeleta mafanikio kwenye zao la mbaazi, wananchi wamepata ongezeko la thamani ya zao hilo lakini pia kuhusu korosho Mhe. Rais amesema Serikali inajenga kongani ya viwanda ili kuongeza thamani ya zao hilo.

“Suluhisho la kupata bei nzuri ya korosho ni kuongeza thamani korosho zetu. Katika kuongeza thamani tunajenga kongani ya viwanda, Maranje ambapo patakuwa na kituo cha kukoboa korosho zote za Mtwara. Korosho zitaongezwa thamani, ili tuuze korosho zilizotengenezwa.Tukiongeza thamani bei itakuwa nzuri”.

Aidha akawakumbusha wananchi wa Masasi kutumia fedha kwenye mambo yenye tija sambamba na kusisitiza suala la elimu kwa kupunguza tamaduni zinazochochea ongezeko la mimba utotoni.

“Wachezeni wakiwa na umri mkubwa huku wakijua mambo wanayofundishwa” Mhe. Rais Dkt. Samia




Kazi iendelee “ Nataka niwaambie ndugu zangu wa Masasi kwamba, Maendeleo yanakuja kwa vitendo na kwakuchukua hatua mahususi na si kwa maneno. Maendeleo ni vitendo. Ninatoa rai kwa watanzania wote popote walipo kuunga mkono jitihada hizi za Serikali na kufanya kazi kwa bidii. Kama ni mkulima anza sasa kuongeza mashamba, ili mazao yawe mengi zaidi, kwani Serikali imejitoa kukuza kilimo kwa kiasi kikubwa”,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihitimisha ziara yake Mkoani Mtwara katika viwanja vya Boma, Halmashauri ya Mji Masasi.

MICHEZO

## MAPOKEZI YA MABINGWA WA MCHEZO WA MPIRA WA WAVU (VOLLEYBALL) AFRIKA MASHARIKI



Timu ya Mpira wa wavu (Volleyball) ya wanafunzi kutoka shule ya Msingi Kambarage, Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara imeandika historia ya kuwa Mabingwa wa Mashindano ya Michezo kwa shule za sekondari na shule za msingi za nchi za Afrika Mashariki (FEASSSA) yaliyofanyika nchini Rwanda kwa mwaka 2023.



Mashindano hayo yalianza agosti 17 hadi 27, 2023 huku fainali ikipigwa agosti 27 ikihusisha Nchi nne ambazo ni Rwanda, Kenya, Uganda na Tanzania.

Timu kutoka Shule ya Msingi Kambarage ilikuwa ni timu pekee kutoka Tanzania kwa shule za Msingi na imeshinda kwa jumla ya pointi 12.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Wataalam kutoka Halmashauri ya Mji Masasi
wakiwa katika mafunzo ya NeST, Agosti 28-sep 1, 2023 Mtwara



Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Mji Masasi
wapo kidigitali (matumizi ya vishikwambi kwenye vikao).



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Julai 30, 2023 (ukaguzi miradi)
katika picha ya pamoja na wanafunzi wa shule ya sekondari ya wasichana Masasi



Mafuriko ya wananchi wa Masasi Mji wakimpokea
Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan Septemba 16, eneo la TK Masasi.



Wakuu wa Mikoa ya Mtwara na Lindi walipotembelea
banda la Halmashauri ya Mji Masasi agosti 8, 2023 Ngongo-Lindi

***Jarida la Mtandaoni limeandaliwa na,***
***Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***
***Halmashauri ya Mji Masasi***

## VIWANJA ! VIWANJA! VIWANJA

Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Masasi anawatangazia wananchi wote wa Masasi na Nje ya Masasi kuwa Halmashauri Inauza VIWANJA BORA vilivyopimwa kwa Matumizi mbalimbali.

**ENEO**

MAILISITA (BARABARA KUU MASASI-NAMAKOGWA-LINDI)
**KM 6 TU KUTOKA MASASI MJINI**

**BEI**

| Matumizi | Bei kwa Mita Moja ya Mraba |
|---|---|
| MAKAZI PEKEE | SH. 2500 |
| MAKAZI/ BIASHARA | SH. 2700 |
| UWEKEZAJI | SH. 3000 |
| BIASHARA PEKEE | SH. 2700 |
| HUDUMA ZA JAMII | SH. 3000 |

Kwa Mawasiliano na Taratibu za Ununuzi fika
OFISI YA MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI MASASI
AU PIGA SIMU NAMBA, 0783-861-778 EMAIL: info@masasitc.go.tz